

1. Mungu liye hai—
Wa kweli na Muumba
Yehova jina lako—
Halibadiliki.
Tunajivunia
Kuitwa jina lako.
Na duniani kote,
Sifa twatangaza.

(KORASI)

*Yehova, Yehova,
Wewe ndiye Mungu.
Mbinguni na duniani
Hakuna mwingine.
Ni wewe tu Mweza-Yote,
Wote watambue.
Yehova, Yehova,
Hatuna Mungu mwingine.*

2. Watufanya tuwe,
Kile unachotaka,
Yehova jina lako—
Nasi twakutii.
Mashahidi wako
Umetuita hivyo.
Heshima kubwa sana—
Kuwa watu wako.

(Korasi)